



Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

DONDOO ZA MAZUNGUMZO

KUHUSU MPANGO WA UGAWAJI VYANDARUA SHULENI

Mradi wa ugawaji wa vyandarua shuleni unahusu nini?

Ugawaji wa vyandarua shuleni ni sehemu ya mkakati endelevu wa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao lengo lake ni kuhakikisha vyandarua vilivyogawiwa kwenye kampeni ya ugawaji wa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano na kwa kila sehemu ya malazi vinaendelea kuwepo. Ili kuweza kuwa na kiwango kikubwa cha kutosha cha vyandarua na kubadili vyandarua vilivyochakaa kwenye jamii, mpango huu utatumia wanafunzi kama mawakala wa kufikisha vyandarua majumbani. Hii itapelekea kuendelea kuwa na vyandarua zaidi ya asilimia 80 kwenye jamii wakati wote, ambacho ni kiwango muhimu cha kuzuia uambukizaji wa malaria.

Majukumu ya wanafunzi

Vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu vitatolewa bila malipo katika shule zote kila mwaka kwa wanafunzi wote waliosajiliwa katika Darasa la 1, 3, 5, na 7 pia na wanafunzi wa kidato cha 2 na 4. Majukumu ya wanafunzi ni;

- Kuhakikisha wanakuwepo darasani wakati wa uandikishaji kwa ajili ya vyandarua kulingana na watakvoyoelekezwa na mwalimu wao wa darasa.
- Kuwashirikisha wazazi, marafiki na majirani kuhusu mpango wa ugawaji wa vyandarua shuleni.
- Wakipata chandarua hakikishe wanakipeleka nyumbani na kuwakabidhi wazazi.
- Kama kuna chandarua cha ziada kwenye kaya yao, washawishi wazazi wao kuwapa majirani wasie na chandarua.
- Vyandarua vina thamani kubwa sana hivyo vinahitaji matunzo ya kutosha, ambayo yatapelekea kudumu kwa muda mrefu. Shona chandarua chako pindi kinapochanika.

Kwanini wanafunzi?

- Wanafunzi wanapewa vyandarua kwa sababu ni mojawapo ya njia nzuri yenye uwezo wa kufikia idadi kubwa ya kaya.
- Kaya nyingi zina wanafunzi wanaosoma mojawapo ya madarasa yaliyochaguliwa kwa hiyo kaya nyingi zitafikiwa japo na chandarua kimoja kimoja.
- Wanafunzi watatumika kama mawakala wa kupeleka vyandarua kwenye kaya zao na kwa jamii zao kwa ujumla.

Wanafunzi ambao hawatapata vyandarua awamu hii wanatakiwa kufanya nini?

Siyo kila mwanafunzi ataweza kupata chandarua kwa awamu hii. Wanafunzi ambao hawatapata vyandarua awamu hii, watavipata awamu inayofuata wakiingia kwenye madarasa yanayohusika na ugawaji wa vyandarua.

Majukumu ya jamii katika mpango wa ugawaji vyandarua shuleni ni yapi?

- Jamii zifanye kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kaya zote zinapata vyandarua kulingana na mahitaji yake. Hii itafanikiwa endapo kaya zitakazopata vyandarua zaidi ya idadi inayohitajika zitawapatia kaya ambazo hazina vyandarua vya kutosha na pengine hazina kabisa mtoto anayesoma shule ya msingi au sekondari.
- Hakikisha wewe na jirani zako mnajikinga na malaria ili kuweza kuvunja mzunguko wa uambukizaji wa malaria kwenye jamii yako.



Mwanafunzi anapokea chandarua



Mwanafunzi anamkabidhi mzazi chandarua




Familia wamelala kwenye chandarua



Mama akigawa chandarua cha ziada kwa jirani



Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii



malaria haikubaliki